

Bishop Charles Salalah: The great call of God

**MOROGORO : CHUO CHA UJENZI
NOV 10-13, 2009.**

THEOLOJIA YA KIROHO

MWITO MKUU WA MUNGU KATIKA MAISHA YA MTUMISHI

UTANGULIZI

Mungu alimwumba mwanadamu, kwa mfano wake na sura yake ili awe na uhusiano naye. Mwa 1:26-27, 2:8-23. Hili lilkuwa kusudi la Mungu na linaendelea kubaki kuwa kusudi lake hata leo.

Mungu alipoingia katika mahusiano na Abraham, alipenda awe karibu naye kama rafiki: Isa 41:8; Yak 2:23 wakati wote Mungu anatafuta uhusiano wa jinsi hii kwa watu aliowaumba katika mfano wake. Yh 15:14; Kut 33:11.

Tunaweza kusema kuwa uhusiano wetu na Mungu ni jambo muhimu kuliko jambo jingine lolote lile.

Lakini, pia tunaweza kusema kuwa mambo mengine yote tunayoweza kuwa nayo ama kuyafanya yanategemea sana uhusiano tulionao na Mungu. Hivyo basi, katika mada yetu hii tutaanza na kipengele cha uhusiano wetu na Mungu, kitafuatiwa na kipengele cha uhusiano wetu katika ndoa/familia. Kipengele cha tatu kitakuwa huduma tunazotoa kwa wengine. Kwa mfano kuhubiri, kufundisha, kushauri n.k.

Kipengele Cha Kwanza : Uhusiano wetu na Mungu

Mifano mbali mbali ya uhusiano:

- Uhusiano wa baba na mtoto
- Uhusiano wa mume na mke
- Uhusiano wa ‘Boss’ na mtu aliye chini yake
- Uhusiano wa paka na Panya
- Uhusiano wa mtu na rafiki yake

Uhusiano na Mungu

Ni mifano wa uhusiano wa juu na mwezi . Kut 34:29-35, 2 Kor 3:7-16

Uhusiano sahihi na Mungu hutoa matokeo katika maisha ya mwanadamu. Haiwezekani mtu akawa na uhusiano sahihi na Mungu na akawa hana mabadiliko yo yote katika maisha yake.

Uhusiano sahihi na Mungu ni msingi imara katika maisha ya mwanadamu. Uadilifu, uaminifu, uvumilivu na utu wema unatokana na uhusiano sahihi na Mungu, ni sawa na nyumba iliyojengwa juu ya mwamba. Mat 7:24-27.

Wito Mkuu wa Mungu kwa mwanadamu

I Tim 4:11-16, 5:7; Mdo 20 :28

Katika hatua hii kuwa na mjadala juu wito huu katika mazingira halisi tuliyo nayo.

Kipengele cha Pili: Uhusiano katika ndoa/familia zetu.

Ndoa na familia ni taasisi ambazo zimeanzishwa na Mungu mwenyewe. Umuhimu wake ni huo, kwamba Mungu mwenyewe katika hekima yake alianzisha taasisi hizi. Mwa 1:26-28; 2:18-25.

Angalizo : Tamaduni za wanadamu zimeweka mambo mengi juu ya taasisi hizi:- Mengine mazuri na mengine si mazuri. Kanisa la Kristo kwa kulitumia neno la Mungu lina wajibu wa kuziweka taasisi hizi katika makusudi ya Mungu.

Katika hatua hii, wanasemina watakuwa katika vikundi na kujadili suala la athari wanazoziona katika taasisi ya ndoa/familia ambazo zimeletwa na utamaduni wao. Hapa wanaume peke yao kadhalika na wanawake.

Baada ya kupokea taarifa ya vikundi, na kujadili, tutaangalia suala la mwonekano wa ndoa/familia ya kikristo. Hapa tutaongozwa na Neno la Mungu.

Kipengele cha Tatu: Huduma tunazotoa kwa Wengine

Katika sehemu hii tutatumia I Tim 4:11-5:1ff kama msingi wa kuangalia huduma zetu zinavyopaswa kuwa na sisi wenyewe tunavyopaswa kuwa.

Mkazo utawekwa juu ya maisha matakififi kama nguzo na msingi imara wa huduma itakayoleta heshima mbele za Mungu.